

TAARIFA KWA UMMA

WITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA LESENI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MIKUMI

Mnamo tarehe 08 Juni, 2017, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi la kupatiwa leseni kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mikumi (MIKUMI WSSA). Leseni inayoombwa ni ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika mji wa Mikumi.

Mamlaka ya Maji Mikumi ilianzishwa kwa tangazo la serikali namba 29 la tarehe 30 Januari, 2004, na kupewa majukumu ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Mikumi. Ofisi za Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mikumi zipo katika mji mdogo wa Mikumi, uliomo katika Wilaya ya Kilosa. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mikumi iko katika daraja la C la Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira.

Yafuatayo ni maelezo kwa kifupi kuhusu mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira Mikumi;

1.0 Jina na Anuani:

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira MIKUMI
Mtaa wa Kidoma,
Barabara kuu ya Morogoro-Iringa
S.L.P 57,
Mikumi-Morogoro,
Tanzania

2.0 Maelezo ya Leseni:

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira, Mikumi, imeomba leseni ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira mjini Mikumi. Eneo la huduma ambalo, mamlaka inatakiwa ilihudumie ni mjini Mikumi, wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro.

3.0 Miundombinu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira

Vyanzo vya maji vinavyotegemewa na Mamlaka ya Maji Mikumi ni chemchem ya Madibila, yenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 720 za maji kwa siku. Miundombinu ya muombaji, inajumuisha, matanki mawili ya kuhifadhi maji, yaliyojengwa kwa matofali ya saruji, yote kwa pamoja yana uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 360. Aidha, miundombinu hiyo, inajumuisha, mtandao wa kusambaza majisafi wenye urefu wa kilomita 26. Muombaji hana mitambo ya kutibu majisafi, aidha muombaji hana mitambo ya kuondoa na kusafisha majitaka.

4.0 Umiliki

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mikumi, inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Tanzania.

Kulingana na kipengele cha 19(2) cha Sheria ya EWURA, sura ya 414, EWURA imeanzisha mchakato wa kukusanya maoni juu ya uhalali wa maombi hayo ya leseni.

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi tajwa hapo juu afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini kabla ya saa 11 jioni ya tarehe 31 Juni, 2017. Nyaraka za maombi hayo zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote, kwa maombi maalum ya maandishi kwa anuani iliyooneshwa hapa chini.

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji,
Ghorofa ya 7, Jengo la LAPF Pension Fund,
Mkabala Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama
S.L.P 72175, Dar es Salaam,
Simu: +255-(022) 2923513
Nukushi: +255-(022)-2923519
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: www.ewura.go.tz**